# CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO TPS

**(TPS SACCOS LTD)**

**DSR 845**

# MASHARTI YA CHAMA

*Imeandaliwa na Bodi ya*
TPS SACCOS LTD
SLP 78067
DAR ES SALAAM
Simu: (+255)-022-2865223
Email:tpssaccos@prisons.go.tz

**TOLEO LA 2,2020**

**CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO TPS**

**(TPS SACCOS LTD)**

**DSR 845**

# MASHARTI YA CHAMA

*Imeandaliwa na Bodi ya*
TPS SACCOS LTD
SLP 78067
DAR ES SALAAM
Simu: (+255)-022-2865223
Email:tpssaccos@prisons.go.tz

**TOLEO LA 2,2020**

**SHERIA YA VYAMA VYA USHIRIKA**
**(SHERIA Na. 6 YA MWAKA 2013)**

---

**MASHARTI**
**TOLEO LA 2018**
*(Yametungwa chini ya kifungu cha 52)*

---

# MASHARTI YA CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO TPS

# (TPS SACCOS LTD)

## MPANGILIO WA MASHARTI


| Sharti | Kichwa cha matakwa |
|---|---|
| | **SEHEMU YA KWANZA** |
| | **MASHARTI YA AWALI** |
| **1** | Dondoo na Masharti kuanza kutumika |
| **2** | Tafsiri |
| | **SEHEMU YA PILI** |
| | **TAARIFA ZA CHAMA** |
| **3** | Jina la chama |
| **4** | Anuani ya chama |
| **5** | Mfungamano wa Pamoja |
| **6** | Eneo la shughuli za chama |
| **7** | Tarehe ya kusajiliwa namba ya usajili |
| **8** | Mwaka wa fedha |

## SEHEMU YA TATU

## MADHUMUNI


| | |
|---|---|
| **9** | Madhumini ya TPS SACCOS LTD |


## SEHEMU YA NNE

## UANACHAMA


| | |
|---|---|
| **10** | Sifa za uanachama |
| **11** | Maombi ya uanachama |
| **12** | Wanachama wa TPS SACCOS LTD |
| **13** | Kushughulikia maombi ya uanachama |
| **14** | Taarifa ya kukataliwa uanachama |
| **15** | Kiingilio, Hisa na Akiba |
| **16** | Kuteua Mrithi |
| **17** | Kukoma uanachama |
| **18** | Malipo ya haki za mwanachama aliyejitoa au kufukuzwa uanachama |
| **19** | Kusimamishwa na kufutiwa uanachama |
| **20** | Kupokelewa tena kwenye chama |
| **21** | Wajibu wa Mwanachama |
| **22** | Haki za Mwanachama |
| **23** | Stahili za aliyekoma kuwa mwanachama |
| **24** | Dhima ya mwanachama |
| **25** | Ajira katika chama |

## SEHEMU YA TANO

## FEDHA NA MALI ZA CHAMA


**26** Vyanzo vya fedha

**27** Mali za TPS SACCOS LTD

**28** Mali za TPS SACCOS LTD kuwekwa Rehani

**29** Ukaguzi wa hesabu za chama


## SEHEMU YA SITA

## TARATIBU KUHUSU AKIBA, AMANA NA MIKOPO


**30** Chama kuandaa Sera

**31** Uwekaji wa Akiba na Amana

**32** Utunzaji wa kitabu cha mwanachama

**33** Mikopo kwa wanachama

**34** Kamati ya Usimamizi kusimamia utoaji wa mikopo


## SEHEMU YA SABA

## UHIFADHI WA FEDHA ZA CHAMA


**35** Uhifadhi wa fedha za chama


## SEHEMU YA NANE

## MATENGO NA MGAO WA ZIADA


**36** Mfuko wa Matengo ya Kisheria

**37** Mfuko wa Elimu na mafunzo

**38** Mgawo wa ziada halisi

## SEHEMU YA TISA

## USIMAMIZI NA UONGOZI WA CHAMA


| | |
|---|---|
| **39** | Mamlaka ya Mkutano Mkuu |
| **40** | Mkutano Mkuu wa Mwaka |
| **41** | Mkutano Mkuu wa Kawaida |
| **42** | Mkutano Mkuu Maalumu |
| **43** | Notisi ya Mkutano Mkuu |
| **44** | Akidi ya Mkutano Mkuu |
| **45** | Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu |
| **46** | Upigaji Kura katika Mkutano Mkuu |
| **47** | Muhtasari wa Mkutano Mkuu |


## SEHEMU YA KUMI

## BODI YA UONGOZI NA KAMATI YA USIMAMIZI


| | |
|---|---|
| **48** | Bodi ya Uongozi |
| **49** | Kukoma Ujumbe wa Bodi; |
| **50** | Vikao vya Bodi ya Uongozi |
| **51** | Muhtasari wa Vikao vya Bodi ya Uongozi |
| **52** | Kazi za Bodi ya Uongozi |
| **53** | Kazi za Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi |
| **54** | Kazi za Makamu Mwenyekiti |
| **55** | Sifa za Mjumbe wa Bodi ya Uongozi na wa Kamati ya Usimamizi |
| **56** | Kazi za Meneja |
| **57** | Kamati ya Usimamizi |
| **58** | Kazi za Kamati ya Usimamizi |

59 Kamati ya Mikopo

60 Wajibu wa Kamati ya Mikopo

61 Akidi ya Vikao vya Kamati ya Mikopo

62 Rufaa dhidi ya maamuzi ya Kamati ya mkopo

63 **SEHEMU YA KUMI NA MOJA**

**UANDAAJI WA SERA NA MIONGOZO YA CHAMA**

Chama kuandaa sera na miongozo

**SEHEMU YA KUMI NA MBILI**

**KUFUTWA NA UFILISI WA TPS SACCOS LTD**

64 Sababu za kufutwa

65 Ufilisi

**SEHEMU YA KUMI NA TATU**

**MASHARTI MENGINEYO**

66 Viongozi kutunza siri

67 TPS SACCOS LTD kuungana na taasisi nyingine

68 Bima ya mali na fedha za chama

69 Mabadiliko ya Masharti

70 Utatuzi wa migogoro

71 Mgongano wa tafsiri ya Masharti

72 Utakatishaji wa fedha

73 Uombaji wa Leseni

74 Ulinzi wa mtaji

| | |
|---|---|
| **75** | Mihuri ya Chama |
| **76** | Msemaji wa chama |
| **77** | Ulipaji wa riba na gawio |

**SHERIA YA VYAMA VYA USHIRIKA**
**( SHERIA Na. 6 YA MWAKA 2013)**

**MASHARTI**

(*Yametungwa chini ya kifungu cha 52)*

MASHARTI YA TPS SACCOS LTD.

MASHARTI YA AWALI

Dondoo na Masharti kuanza kutumika

1. Masharti haya yatajulikana kama Masharti ya TPS SACCOS LTD na yataanza kutumika mara baada ya kuidhinishwa na kusajiliwa na Mrajis

Tafsiri

2. Katika Masharti haya, isipokuwa kama muktadha unahitaji vinginevyo:

a) **Afisa Mikopo:-** ni mtu aliyeajiriwa na TPS SACCOS LTD kwa ajili ya kupitia na kuchambua maombi ya mikopo yanayowasilishwa na wanachama na kufanya ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo hiyo.

b) **Akiba**:- Ni kiasi cha fedha kinachowekwa na mwanachama kwa muda fulani kwa ajili ya kupata faida kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa, na fedha hiyo inaweza kuchukuliwa au kutumika kama dhamana ya kupata mkopo.

c) **Akidi:** maana yake ni idadi ya chini au toshelezi ya wajumbe wanaotakiwa kuhudhuria ili kikao au mkutano uwe halali.

d) **Amana**: Ni fedha ambayo mwanachama anaweka katika chama chake kila anapokuwa na fedha ambayo haihitaji kuitumia kwa wakati huo na fedha hiyo inaweza kuchukuliwa au kutumika kama dhamana ya mkopo; pia mwanachama huruhusiwa kuichukua muda wowote wa kazi.

e) **Bodi ya Uongozi:** maana yake ni Bodi ambayo imechaguliwa na

Mkutano Mkuu kwa ajili ya kusimamia shughuli za kila siku za chama.

f) **Chama** maana yake ni Ushirika wa Akiba na Mikopo kwa Watumishi wa Jeshi la Magereza Tanzania Bara (TPS SACCOS LTD) na wenza wao.

g) **Dhamana**: Ni kinga kwa ajili ya mkopo uliochukuliwa, inaweza kuwa nyumba, shamba, vyombo, Hisa za hiari, Amana, Akiba au mali nyingine itakayokubalika kutumika kwa madhumuni hayo.

h) **Hisa :** ni sehemu ya umiliki wa mtaji wa chama ambayo inaweza kumilikiwa na mwanachama lakini haitakiwi kuzidi asilimia ishirini ya mtaji hisa wa chama;

**Hisa za hiari:** maana yake ni fedha zinazoweza kuchukuliwa na zinaweza kutumiwa na mwanchama kama dhamana kwa kuzingatia vigezo na masharti yaliyomo katika Sera ya uhamasishaji wa hisa;

i) **Kanuni:** ina maana ya Kanuni za Vyama vya Ushirika ya mwaka 2015;

j) **Kanuni za SACCOS:** ina maana Kanuni za Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo ya mwaka 2014 na Marekebisho yake ya Mwaka 2018, na kanuni za jumla za Vyama vya Ushirika za Mwaka 2015.;

k) **Afisa:** maana yake ni mtu mwenye wadhifa wa kuchaguliwa au kuajiriwa katika TPS SACCOS LTD ambaye atajumuisha Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wa Bodi, Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi, Mjumbe Mwakilishi, Meneja Mkuu, Mhasibu Mkuu, Mkaguzi wa Ndani, Mhazini na Wajumbe wengine waliopewa mamlaka chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika.

l) **Mfungamano wa Pamoja:** maana yake ni jamii inayolengwa na chama ambayo ndio itakayotoa wanachama wa chama husika.

m) **Mrajis:** maana yake ni kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Vyama

vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013.

n) **Sera ya Mikopo**: maana yake ni utaratibu au mwongozo uliowekwa na wanachama kuongoza watendaji wa TPS SACCOS LTD katika shughuli zinazohusiana na mikopo ili kufikia malengo yaliyowekwa kwa manufaa ya wanachama.

o) **Sheria:** ina maana Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013.

p) **TPS SACCOS LTD** maana yake ni Chama cha Akiba na Mkopo cha watumishi wa Jeshi la Magereza Tanzania bara na wenza wao.

q) **Tume:** ina maana Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 HISTORIA YA CHAMA

TPS SACCOS LTD ni Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo kwa watumishi wa Jeshi la Magereza na wenza wao, kilichosajiliwa Agosti 11, 2005 na kupewa Hati Na. DSR. 845. Chama hiki kilianza na Wanachama wapatao 80 na mtaji wa TShs. 8,000,000/= kikiwa chini ya mlezi wa Chama EX- PCP **NICAS PIUS BANZI**. Lengo hasa ni kuboresha maisha ya askari kwa kutoa Mikopo yenye riba nafuu na kuwawezesha kujiwekea akiba katika mazingira salama.

## 1.1 DIRA (MISSION)

Malengo yanayokusudiwa na TPS SACCOS Ltd ni kuinua na kuendeleza Wanachama wake kwa kutoa huduma za kifedha na bidhaa mbalimbali katika mazingira ya kiushindani.Pia kuwawezesha Wanachama kuondoa umaskini, kuheshimika na kutambulika chini ya misingi ya ushirika na kibiashara.

## 1.2 DHAMIRA

Ili kufikia malengo ya kuanzishwa kwake,TPS SACCOS Ltd itaendeshwa kwa kuzingatia Dira ifuatayo;-

a) Kuwa Asasi bora ya Ushirika wa Akiba na Mikopo yenye kutoa bidhaa na huduma madhubuti za kifedha zinazohitajika na kutumiwa na Wanachama wake;
b) Kuwa na Viongozi, Wanachama na Watendaji wenye ujuzi na uwezo wa kuendesha TPS SACCOS Ltd kihuduma na kibiashara.

## 1.3 MAADILI (CORE VALUES)

Mwenendo wa Ushirika wa Akiba na Mikopo wa Watumishi wa Jeshi la Magereza Tanzania Bara umejengeka katika maadili ya kusaidiana,kuwajibika,Demokrasia,Usawa na Haki.Wanachama wanaamini katika maadili ya Ukweli,Uwazi,Uaminifu,Uwajibikaji kijamii na kuwasaidia wengine.

## 1.4 MAREJEO YA MASHARTI

- Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013 na kanuni zake;
- Sheria ya Huduma ndogo za fedha za, 2018 na kanuni zake.
- Sera mbalimbali za Chama

- Mpango Mkakati wa Chama
- Maamuzi ya Wanachama kupitia Mkutano Mkuu
- Mpango Biashara

## 1.5 WIGO WA MASHARTI YA TPS SACCOS LTD

**(a) Wadau wa ndani**

(i) Wanachama
(ii) Viongozi wa Bodi na Kamati zake
(iii) Wafanyakazi/Watendaji

**(b) Wadau wa nje**

i) Wakaguzi wa nje
ii) Maafisa Ushirika
iii) Taasisi za Kifedha na wakopeshaji wengine

# SEHEMU YA PILI

## TAARIFA ZA CHAMA

Jina la chama

3. Jina la chama ni TANZANIA PRISONS SAVING AND CREDIT COOPERATIVE SOCIETY LTD.

Anuani ya chama

4. (i) Anuani ya Chama ni S.L.P.78067, DAR ES SALAAM.

(ii) Mabadiliko yoyote ya anuani, eneo la Ofisi ya Chama ni lazima yatolewe taarifa kwa maandishi kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika na mabadiliko hayo hayatasababisha marekebisho ya Masharti ya Chama.

Mfungamano wa Pamoja

5. Mfungamano wa pamoja katika TPS SACCOS LTD utakuwa ni kuwa Mtumishi wa Jeshi la Magereza, Mwenza wa Mtumishi wa Jeshi la Magereza au mtumishi mstaafu aliyekuwa Mwanachama na ameamua kwa hiari yake kuendelea kuwa Mwanachama,Watumishi wa taasisi nyingine za Serikali, na Watendaji wa Chama.

Eneo la shughuli za TPS SACCOS LTD.

6. Eneo la shughuli za TPS SACCOS LTD litakuwa ni KEKO MAGEREZA BARABARA YA MAENDELEO MTAA WA MAENDELEO WILAYA YA TEMEKE MKOA WA DAR ES SALAAM.

Tarehe ya kusajili

7. TPS SACCOS LTD imesajiliwa tarehe 11 Agosti 2005 na kupewa Hati Na. DSR. 845.

Mwaka wa fedha

8. Mwaka wa fedha wa TPS SACCOS LTD utakuwa ni kipindi cha miezi kumi na mbili kuanzia tarehe moja ya mwezi Januari na kukomea tarehe thelathini na moja ya mwezi Desemba ya mwaka husika.

TANZANIA
Registered this 01ST
day of MARCH 2021
Asst. Registrar of Cooperative Societies

## SEHEMU YA TATU

## MADHUMUNI

Madhumuni ya TPS SACCOS LTD

9. Madhumuni ya kuanzishwa kwa TPS SACCOS LTD ni kuinua, kuimarisha na kuendeleza hali ya kiuchumi na kijamii ya wanachama wake kwa kufuata Sheria, Kanuni na taratibu za Vyama vya Ushirika. Ili kufanikisha madhumuni haya, TPS SACCOS LTD itafanya yafuatayo:-

a) Kuhamasisha wanachama wake kujenga tabia ya kujiwekea Akiba mara kwa mara.

b) Kupokea na kutunza Akiba na Amana za wanachama kwa njia rahisi na salama huku ikilipa riba kadri Wanachama watakavyokubaliana.

c) Kutafuta vyanzo vya fedha ili kujenga na kuimarisha mtaji kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanachama kwa masharti na riba nafuu.

d) Kuwaelimisha wanachama kujijengea tabia ya kukopa kwa busara na kutumia vizuri mikopo kwa ajili ya kuinua hali zao za maisha kiuchumi na kijamii.

e) Kubuni na kutoa bidhaa mbalimbali za kifedha kwa wanachama ili waweze kushiriki zaidi katika kuimarisha mtaji wa chama na mitaji yao binafsi na kuleta mvuto kwa wasio wanachama kujiunga na chama.

f) Kuweka kwa usalama fedha za chama kwa kuanzisha mipango ya kukabiliana na majanga.

g) Kuwashauri wanachama kuandaa mipango yao ya maendeleo katika kuwekeza mitaji kwenye miradi ya kiuchumi na huduma za jamii.

h) Kuhifadhi ziada katika mashirika ya fedha au kununua hisa na kuweka dhamana kwenye vyombo vya fedha, serikali na kwenye makampuni yanayoendesha shughuli zake kwa faida.

i) Kuhakikisha fedha na mali nyingine za wanachama zinahifadhiwa mahali penye usalama wa kutosha na wa uhakika kwa kupanga utaratibu unaofaa wa kutunza na kuweka kinga ya mikopo.

j) Kushirikiana na wakala mbali mbali na vyama vingine vya ushirika

vinavyoendesha shughuli za kuweka Akiba na Mikopo kwa lengo la kuwawezesha wanachama kujikwamua kiuchumi na kijamii na kuimarisha mtaji wa kukopeshana.

k) Kuwahamasisha wasio wanachama kujiunga na chama.

l) Kutoa elimu kwa wanachama kuhusu dhana ya ushirika na manufaa yake, ujasiriamali na tasnia nyingine zinazohusiana na miradi inayoendeshwa na kutekelezwa na wanachama wake.

m) Kufanya mambo mengine ambayo yataimarisha na kuendeleza hali ya uchumi wa chama na wanachama.

n) Kuweka viwango vya faida juu ya Akiba, Amana na riba ya mikopo ya Wanachama vinavyokidhi gharama za uendeshaji na kuleta manufaa kwa chama na Wanachama.

## SEHEMU YA NNE

## UANACHAMA

Sifa za uanachama

10. Mtu yeyote anaweza kuwa mwanachama akiwa na sifa zifuatazo:

a) Awe raia wa Tanzania mwenye umri usiopungua miaka kumi na nane

b) Awe na akili timamu;

c) Awe muadilifu;

d) Awe mtumishi wa jeshi la magereza, mume au mke au mtumishi mstaafu aliyekuwa mwanachama na ameamua kwa hiari yake kuendelea kuwa mwanachama,mtendaji wa chama,watumishi wa idara mbalimbali za serikali.

e) Awe tayari kushiriki kikamilifu katika shughuli zote za chama.

f) Asiwe na shughuli binafsi zinazofanana na shughuli za chama.

g) Awe amelipa kiingilio na kununua hisa kwa kadiri inavyotakiwa na Masharti haya.

h) Awe tayari kufuata masharti ya chama, kanuni na Sheria za Vyama Vya Ushirika inayotumika kwa kipindi hiki.

Maombi ya uanachama

11. Maombi ya uanachama baada ya chama kusajiliwa yatafanywa kwa utaratibu ufuatao:

a) Mwombaji atajaza fomu ya uanachama na kupitishwa na Bodi na baadaye kuidhinishwa na Mkutano Mkuu.

b) Mwombaji atapaswa kununua Masharti ya chama kwa shilingi elfu kumi (10,000/-) au kiwango kingine kitakachoidhinishwa na Mkutano Mkuu na kuyasoma kikamilifu ili kuelewa madhumuni ya chama, wajibu na haki zake.

c) Fomu ya maombi ya uanachama itakuwa na maelezo ambayo yatakuwa na saini ya mwombaji kama uthibitisho kuwa amesoma Masharti haya na anakubali kuyatii.

d) Fomu ya maombi ya uanachama italipiwa shilingi 10,000/= (elfu Kumi) au kiwango kingine ambacho kitapangwa na kuidhinishwa na Mkutano Mkuu.

Wanachama wa TPS SACCOS LTD.

12. Wanachama wa TPS SACCOS LTD watatokana na:-

a) Wale wote walioshiriki katika mchakato wa uanzilishi na kuomba kuandikishwa kwa chama na ambao wametimiza masharti ya uanachama kwa mujibu wa Masharti haya; na

b) Wale wote watakaojiunga na chama baada ya kukubaliwa na Bodi na kupitishwa na Mkutano Mkuu.

Kushughulikia maombi

13. Maombi na uthibitisho wa uanachama utafuata utaratibu ufuatao:-

ya uanachama

a) Mtu yeyote atakayekuwa ametimiza sharti Na.10 na kuomba uanachama kwa kujaza fomu iliyoandaliwa na Chama, anaweza kujadiliwa na kukubaliwa/kukataliwa na Bodi ya Uongozi ya chama kuwa mwanachama.

b) Pendekezo la Bodi ya Uongozi litapelekwa mbele ya Mkutano Mkuu kwa uthibitisho ambapo waombaji wote wanayo haki ya kuhudhuria Mkutano Mkuu huo na kusikilizwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu na uamuzi wa Mkutano Mkuu utakuwa wa mwisho.

c) Mwombaji atakapokubaliwa na Bodi atatakiwa kulipa kiingilio na Hisa na baada ya kupokelewa na Mkutano Mkuu atatakiwa kutia saini yake au kuweka dole gumba katika daftari la wanachama mbele ya wajumbe wa Bodi wawili;

d) Mwanachama akishapitishwa na Mkutano Mkuu atakuwa na haki ya kupatiwa kitambulisho cha uanachama na endapo kitambulisho kitapotea, mwanachama atapewa kitambulisho kingine kwa kulipa gharama ya shilingi elfu kumi (10,000/=) au kiwango kingine kitachachowekwa na kuidhinishwa na Mkutano Mkuu.

Taarifa ya kukataliwa uanachama

14. Endapo maombi ya kujiunga na chama yamekataliwa na Bodi ya Uongozi:-

a) Bodi ya Uongozi itapaswa kumwandikia mwombaji barua ya kumjulisha kuhusu kukataliwa kwa maombi yake ikieleza sababu za kukataliwa na kurudishiwa fedha za kiingilio na Hisa zote zilizopokelewa kutoka kwa mwombaji huyo; na

b) Mwombaji ambaye maombi yake yamekataliwa na Bodi ya Uongozi anaweza kukata rufaa kwa maandishi kwa Mkutano Mkuu kupitia kwa Afisa Ushirika wa eneo husika ambaye ataiwasilisha kwenye Mkutano Mkuu ambao utatoa uamuzi wa mwisho.

Kiingilio, Hisa na Akiba

15. (1) Mwanachama atakapokubali kujiunga na Chama atapaswa:-

a) Kulipa kiingilio cha shilingi elfu kumi. (10,000/=);

b) Kununua hisa ishirini (10) zenye thamani ya shilingi elfu kumi na tano (15,000/=) kwa kila hisa na ili awe mwanachama atapaswa kununua na kulipia kikamilifu angalau hisa Kumi (5) na hisa kumi (5) zilizobaki atapaswa kuzilipia katika kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili(12); na

c) Kuweka Akiba kila mwezi isiyopungua shilingi elfu ishirini (20,000/=) Kwa ajili ya maisha ya baadaye na pia anaweza kuitumia kama dhamana ya kukopea.

(2) Viwango vya kiingilio, hisa na akiba vinaweza kubadilishwa kwa maamuzi ya Mkutano Mkuu.

(3) Mwanachama aliyekamilisha kulipia Hisa zote atapewa hati ya kumiliki Hisa.

(4) Mwanachama atakaye shindwa kununua hisa kufikia kiwango cha chini katika muda uliopangwa, atasimamishwa uanachama. Kabla ya mkutano wa TPS SACCOS LTD haujachukua hatua hiyo, mwanachama atapewa taarifa ili achukue hatua za kukamilisha ununuzi wa hisa husika.

Kuteua Mrithi

16. (1) Mwanachama atamteua mrithi wake ambaye atakuwa na haki ya kulipwa hisa au maslahi mengine katika Chama.

(2) Mwanachama atakuwa na haki ya kubadilisha jina la mrithi.

(3) Kila uteuzi wa mrithi utaandikwa katika daftari la wanachama na utatiwa saini na mwanachama.

Kukoma uanachama

17. Uanachama utakoma kwa:-

a) Kupatikana na hatia kwa kosa la wizi au ufujaji wa mali za TPS SACCOS LTD.

b) Kufanya kitendo chochote kinachoathiri maslahi ya TPS SACCOS LTD.

c) Kujiuzulu baada ya kutoa taarifa ya maandishi kwa Bodi ya Chama kwa muda usiopungua siku sitini (60);

d) Kufukuzwa na wanachama katika Mkutano Mkuu kwa idadi ya wanachama wasiopungua theluthi mbili (2/3) ya waliohudhuria na kupiga kura baada ya kupewa nafasi ya kujitetea;

e) Kutenda kosa lolote ambalo limetajwa katika Sheria ya Vyama Vya Ushirika iliyopo na Kanuni zake na Masharti ya Chama;

f) Kuacha kuwa na Hisa kwa mujibu wa masharti haya;

g) Kutohudhuria kwenye Mkutano Mkuu mitatu kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo pasipo kutoa taarifa ya maandishi kwa njia ya barua au barua pepe;

h) Kupatwa na kichaa kilichothibitishwa na Daktari stahiki;

i) Kutoa rushwa kwa Afisa au mtumishi wa chama kwa nia ya kupata upendeleo au kupokea rushwa;

j) Kifo.

Malipo na haki za mwanachama aliyejitoa au kufukuzwa uanachama

18. Mwanachama aliyejitoa au kufukuzwa uanachama atalipwa haki zake zote baada ya kupita kipindi cha miezi miwili kuanzia siku ya kukoma uanachama baada ya kuthibitika kwa haki hizo na kulipa madeni yote anayodaiwa kwenye chama.

Kusimamishwa na kufutiwa uanachama

19. (1) Mwanachama anaweza kusimamishwa uanachama kutokana na:-

a) Sababu zilizotajwa katika kanuni ya 39 (2) ya Kanuni za Vyama Vya Ushirika za mwaka 2015;

b) Kushindwa kurejesha mkopo kwa muda uliopangwa bila ya sababu yoyote inayokubalika;

c) Kushindwa kuweka Akiba kama ilivyoelezwa katika Masharti ya Chama na Sera ya Akiba na Mikopo.

(2) Kabla ya kumsimamisha mwanachama uanachama, Menejimenti ya chama itapaswa kumwandikia Notisi ya kusudio la kumsimamisha uanachama mwanachama husika ikieleza sababu ya kusudio hilo na kumtaka kutoa maelezo ndani ya muda wa siku thelathini ya kwanini kusudio hilo lisitekelezwe.

(3) Menejimenti ya chama itapaswa kuwasilisha kwenye kikao cha Bodi kinachofuata taarifa ya mapendekezo ya kusimamishwa uanachama pamoja na utetezi wa mwanachama husika ambapo Bodi ya Uongozi itapitia, kujadili na kutoa maamuzi

(4) Bodi ya Uongozi ikiazimia kumsimamisha mwanachama itaelekeza Meneja/Katibu wa chama kumwandikia mwanachama husika barua ya kumtaarifu kuhusu kusimamishwa kwake kusubiri maamuzi ya Mkutano Mkuu.

(5) Bodi ya Uongozi itawasilisha taarifa ya kusimamishwa uanachama kwenye Mkutano Mkuu pamoja na mapendekezo yake na Mkutano Mkuu utapaswa kujadili na kutoa maamuzi ya kusimamishwa, kufutiwa uanachama au kubatilisha maamuzi ya Bodi.

(6) Baada ya uamuzi wa Mkutano Mkuu, Bodi ya Uongozi itapaswa kumjulisha mwanachama husika kwa maandishi kuhusu maamuzi hayo

katika muda usiozidi siku saba tangu tarehe ya maamuzi.

(7) Mwanachama ambaye hataridhika na maamuzi ya Mkutano Mkuu atakuwa na haki ya kukata rufaa kwa Mrajis Msaidizi wa Mkoa ndani ya muda wa siku thelathini tangu tarehe ya kupokea taarifa ya maamuzi ya Mkutano Mkuu.

Kupokelewa tena kwenye chama

20. Mwanachama aliyejiuzulu/aliyefukuzwa anaweza kukubaliwa na kupokelewa tena kujiunga na chama baada ya kutuma maombi kwa kufuata masharti haya na baada ya kulipa madeni yote aliyokuwa anadaiwa wakati anakoma kuwa mwanachama

Wajibu wa Mwanachama

21. Wajibu wa mwanachama wa TPS SACCOS LTD utajumuisha:-

a) Kulipa kiingilio cha uanachama, kununua hisa, kuweka Akiba na Amana pamoja na kukopa kwa mujibu wa sera ya mikopo na masharti ya TPS SACCOS LTD.

b) Kuheshimu mikataba ikiwa ni pamoja na kurejesha mkopo na riba katika muda uliopangwa

c) Kurejesha mkopo alioudhamini endapo mkopaji atashindwa kulipa mkopo wake kama alivyoahidi bila sababu ya msingi

d) Kuwa mwaminifu na mwadilifu katika TPS SACCOS LTD.

e) Kuhudhuria mikutano yote ya TPS SACCOS LTD na kushiriki katika utoaji wa maamuzi kwa manufaa ya chama

f) Kuwa na moyo wa kushirikina na wanachama wenzake

g) Kushiriki kikamilifu katika shughuli na miradi ya chama kwa hali na mali ili kuongeza tija katika chama

h) Kuhudhuria mafunzo mbali mbali na elimu ya ushirika na biashara yatakayoendeshwa kwa manufaa ya chama

i) Kutumia huduma zitolewazo na chama kama zilivyoainishwa kwa mujibu wa masharti na madhumuni ya chama.

j) Kuzingatia sheria, kanuni, miongozo, maazimio, ya mikutano mikuu, maadili, sera na taratibu mbali mbali za uendeshaji na usimamizi wa shughuli za chama

k) Kutunza na kulinda mali za chama

l) Kubeba dhamana endapo chama kitapata janga lolote;

m) Kudhamini mkopo wa mwanachama mwenzake isipokuwa kwamba mwanachama aliyemdhamini hatakuwa na haki ya kudhaminiwa na mwanachama aliyemdhamini katika kipindi kile kile;

n) Kulipa mkopo alioudhamini endapo mdhaminiwa/mkopaji atashindwa kulipa mkopo wake;

Haki za Mwanachama

22. Mwanachama wa TPS SACCOS LTD atakuwa na haki zifuatazo:

i) Kupewa taarifa za maendeleo na huduma za chama ikiwa ni pamoja na kupewa nakala za sheria na kanuni za vyama vya ushirika, masharti, kutazama mizania, muhtasari wa mikutano mikuu na nyaraka za mrajis.

ii) Kukata rufaa endapo hataridhika na maamuzi

iii) Kushiriki kikamilifu katika shughuli za Chama na kuhudhuria mikutano yote inayohusika;

iv) Kushiriki katika kutoa uamuzi wa mambo mbalimbali katika Mikutano Mikuu;

v) Kupiga kura chini ya misingi ya mtu mmoja kura moja bila kujali idadi ya Hisa anazomiliki;

vi) Kuchagua na/au kuchaguliwa katika Uongozi wa chama.

vii) Kuwa na haki sawa kuhusu mali ya Chama na kudhibiti ipasavyo matumizi yake;

viii) Kupatiwa huduma zozote zinazotolewa na chama ilimradi amekidhi masharti yanayoambatana na huduma hiyo;

ix) Kupatiwa taarifa mbalimbali za shughuli za chama, muhtasari wa mkutano na nyaraka nyingine za chama kwa ajili ya mapitio akiwa katika ofisi za chama;

x) Kuitisha Mkutano Mkuu kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika na Kanuni zake pamoja na masharti haya;

xi) Kuteua Mrithi;

xii) Kukata rufaa dhidi ya maamuzi ya Bodi ya Uongozi na Mkutano Mkuu;

xiii) Kupokea gawio na faida nyingine kutoka katika shughuli za chama kwa kuzingatia masharti; na

xiv) Kupewa kitabu cha Akiba au kifaa kingine chenye makusudi hayo.

xv) Kufanya malinganisho ya miamala iliyoko kwenye kitabu cha kumbukumbu zake na taarifa zilizopo kwenye vitabu vya chama.

Stahili za mwanachama aliyekoma kuwa mwanachama

23. Stahili za mwanachama aliyekoma uanachama kutokana na sababu zilizotajwa katika kipengele namba 17 cha masharti haya, zinaweza kutumika kama ifuatavyo:-

i) Kulipia mikopo na gharama zingine ambazo mwanachama anadaiwa na Chama;

ii) Bakaa kulipwa kwa mwanachama mwenyewe au kwa mrithi wake aliyeainishwa katika daftari la wanachama; na

iii) Iwapo mwanachama huyo hajulikani alipo na hakuna mrithi au mwakilishi wa kisheria wa mwanachama huyo bakaa ya maslahi yake

yatatumika kwa mujibu wa kanuni ya 37 (6) ya Kanuni za Vyama vya Ushirika.

Dhima ya mwanachama

24. Dhima ya mwanachama kwa madeni ya chama itakuwa ni ya ukomo kwa kiwango cha thamani ya Hisa zake katika chama ambayo hajailipia.

Ajira katika chama

25. (1) Chama kitaajiri au kuazima watu wenye ujuzi unaotakiwa katika kutekeleza kazi za chama kama:-

a) Menejimenti na utawala;

b) Uhasibu/kuandika vitabu vya hesabu;

c) Kutoa na kufuatilia mikopo; na

d) Kazi za muda maalumu.

(2) Watumishi wanaoweza kuajiriwa au kuazimwa ni pamoja na Meneja, Mhasibu, Mkaguzi wa Ndani, Afisa Mikopo, Wanasheria, au watu wengine kadri itakavyohitajika.

## SEHEMU YA TANO

## FEDHA NA MALI ZA CHAMA

Vyanzo vya fedha

26. Fedha za chama zitatokana na:-

a) Kiingilio, Ada, mauzo ya masharti na fomu mbalimbali na michango maalum kutoka kwa wanachama;

b) Hisa za uanachama;

c) Riba juu ya mikopo kwa wanachama;

d) Mikopo kutoka benki, Asasi nyingine za fedha na mifuko ya hifadhi za jamii;

e) Misaada na ruzuku kutoka kwa watu binafsi, taasisi na Asasi nyingine;

f) Ziada halisi ya Chama;

g) Fedha za Akiba ya lazima na malimbikizo ya Ziada;

h) Akiba, hisa za hiari na Amana za wanachama na wasio wanachama; na

i) Mapato mengineyo halali.

Mali za TPS SACCOS LTD

27. Mali za TPS SACCOS LTD zitakuwa ni pamoja na:-

a) Fedha taslimu mkononi na fedha taslimu zilizopo Benki;

b) Uwekezaji katika taasisi mbalimbali;

c) Vifaa na zana zote za chama; na

d) Majengo na mali nyingine za chama kama zilivyooneshwa kwenye daftari la mali za chama.

Mali za TPS SACCOS LTD kuwekwa Rehani

28. Mali za TPS SACCOS LTD zitawekwa rehani kwa idhini ya Mkutano Mkuu.

Ukaguzi wa hesabu za Chama

29. Kila mwisho wa mwaka wa fedha hesabu za chama zitakaguliwa na shirika la ukaguzi na usimamizi wa vyama vya ushirika (COASCO) au Kampuni au mkaguzi mwingine atakayependekezwa na wanachama na kuidhinishwa na mrajisi.

# SEHEMU YA SITA:

# TARATIBU ZA AKIBA, HISA ZA HIARI, AMANA NA MIKOPO

Uwekaji wa Akiba, Hisa za Hiari na Amana

30. (1) Kila mwanachama atatakiwa kuweka Akiba kila mwezi ya kiasi kisichopungua shilingi elfu hamsini (50,000/-) au kiasi kingine kadiri itakavyoamuliwa na Mkutano Mkuu.

(2) Chama kitapokea Hisa za Hiari kutoka kwa wanachama

(3) Akiba ya mwanachama na Hisa za Hiari zinaweza kutumika kama dhamana ya mkopo na Akiba itakuwa ni mojawapo ya kigezo cha kupata mkopo kwa mwanachama.

(4) Chama kitapokea Amana kutoka kwa wanachama na watu wasio wanachama kwa utaratibu utakaokuwa umeainishwa katika sera ya uhamasishaji wa uwekaji Hisa, Akiba na Amana.

(5) Akiba, Hisa za Hiari na Amana za wanachama zitatunzwa sehemu ya usalama na sehemu kubwa zitawekwa benki

(6) Mwanachama anaweza kupunguza Akiba au kuchukua Amana yake kwa kufuata taratibu zilizowekwa na Chama kwenye Sera husika.

(7) Faida juu ya Akiba na Amana zitalipwa kwa kiwango kilichoainishwa kwenye Sera husika au kiwango kingine kitakachopitishwa na Mkutano Mkuu.

Utunzaji wa kitabu cha mwanachama

31. (1) Kila mwanachama atapewa kitabu cha Akiba (passbook) ambacho kitafanyiwa maingizo ya miamala mbalimbali inayomhusu mwanachama.

(2) Kitabu ni mali ya mwanachama, atatakiwa kukionesha wakati wowote anapofanya muamala.

(3) Endapo mwanachama atapoteza kitabu cha Akiba, anatakiwa kutoa

taarifa kwenye chama na kupatiwa kitabu kingine kwa kulipia kiasi cha shilingi elfu tano (5,000/-) au kiasi kingine kitakachoidhinishwa na Mkutano Mkuu.

(4) Mwanachama anatakiwa kutunza kitabu chake na haruhusiwi kufanya maingizo ya muamala wowote yeye mwenyewe.

(5) Endapo mwanachama atafanya maingizo ya muamala wowote mwenyewe atakuwa ametenda kosa la jinai na atapaswa kushtakiwa kwa mujibu wa Sheria ya Makosa ya Jinai.

Mikopo kwa wanachama

32. (1) Mikopo itatolewa kwa wanachama tu kadri ya mahitaji yao kwa kufuata taratibu zilizowekwa na Chama katika sera ya mikopo na italipwa kwa mwanachama kwa hundi iliyofungwa. (Kupitia kwenye akaunti ya mwanachama),isipokuwa kwa mikopo ya dharura inaweza kutolewa kwa taratibu zitakazokuwa zimeainishwa kwenye sera ya mikopo.

(2) Chama kitaanza kutoa mikopo kwa wanachama baada ya kiwango cha chini cha hisa kufikiwa na kukusanya mtaji wa kutosha wa kukopeshana kutokana na Akiba na Amana za Wanachama.

(3) Mwanachama mpya ataruhusiwa kukopa baada ya muda wa miezi mitatu (3) tangu kujiunga na chama.

(4) Kila mwanachama atatakiwa kuonesha kitabu chake cha Akiba (passbook) wakati wa kuomba mkopo, ambacho kitafanyiwa maingizo ya mkopo aliochukua na riba, marejesho (repayments) na kuonesha salio.

(5) Fomu maalumu ya maombi ya mkopo itajazwa na kila mwombaji na kuiwasilisha kwa Afisa Mikopo.

(6) Maombi yote ya mikopo yataidhinishwa na Kamati ya Mikopo, au Kamati ya Kitaalamu. Utoaji wa mikopo utazingatia taratibu, Sera ya Mikopo na Masharti ya Chama.

(7) Gharama za kuandaa mkopo zitakuwa kama zilivyoainishwa kwenye Sera ya Mikopo.

(8) Mwanachama ataruhusiwa kupewa mkopo usiozidi mara tatu (3) ya Akiba zake pasipo kuathiri matakwa ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 na Kanuni zake.

(9) Kamati ya mikopo itawasilisha taarifa za utoaji, ulipaji na madeni ya mikopo kuhusu wanachama kwenye Bodi kila robo ya mwaka.

(10) Kwa mujibu wa Sheria ya Vyama Vya Ushirika na Kanuni zilizowekwa, pamoja na masharti na maazimio yatakayo tolewa na Mkutano Mkuu, Sera ya Mikopo itaainisha dhamana kwa kila mkopo na masharti yatakayotumika katika ulipaji.

(11) Ikiwa fedha za kuwakopesha waombaji wa mikopo hazitoshi, na sababu za maombi zinafanana, maombi ya mikopo midogo midogo yatafikiriwa kwanza na dhamana zionyeshwe katika fomu ya maombi ya mkopo na hati ya ahadi.

(12) Mikopo inaweza kutolewa kwa wanachama kwa njia ya vifaa badala ya fedha taslimu ikiwa thamani ya vifaa hivyo itaweza kujulikana pasipo mashaka kwa pande zote mbili.

(13) Mwanachama anayeomba mkopo atadhaminiwa na wanachama wawili (2) au zaidi kama itakavyoelezwa kwenye Sera ya Mikopo ya Chama.

(14) Mali inayohamishika au isiyohamishika, itakayowekwa dhamana na mkopaji itakuwa chini ya chama mpaka hapo mkopo wote utakapokuwa umelipwa.

(15) Endapo mkopo unahusisha dhamana, dhamana hiyo itapaswa kuhodhiwa na TPS SACCOS LTD na kuwekwa vizuri katika kumbukumbu na kusajiliwa ili kuipa TPS SACCOS LTD uwezo wa kumiliki dhamana hiyo kisheria, kama

italazimu

(16) Urejeshwaji wa mikopo utafanywa kwa njia ya makato kwenye mishahara kwa mujibu wa makubaliano na mwajiri au pesa taslimu kupitia benki

(17) Kamati ya mikopo itapaswa kutoa taarifa kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka kuhusu ufanisi wa shughuli za utoaji, ulipaji na urejeshaji wa madeni ya mikopo.

Kamati ya Usimamizi kusimamia utoaji wa mikopo

33. Kamati ya Usimamizi itasimamisha utoaji wa mikopo katika chama iwapo:-

(i) Mikopo mibaya inazidi asilimia 5% ya jumla ya mikopo iliyotolewa; na

(ii) Bodi haijatoa taarifa ya fedha na takwimu (financial and statistical reports) ndani ya muda unaotakiwa kwa mujibu wa Kanuni za Vyama vya Ushirika na Masharti haya.

## SEHEMU YA SABA

## UHIFADHI WA FEDHA ZA CHAMA

Uhifadhi wa fedha za chama

34. (1) Fedha za chama zitahifadhiwa katika taasisi za fedha.

(2) Kanuni za Fedha za chama zitaainisha kiwango ambacho kinaweza kuchukuliwa kutoka benki na kutunzwa kwenye ofisi za chama kama fedha taslimu mkononi

(3) Malipo yote ya kawaida na yanayozidi shilingi laki tano (500,000/-) yafanywe kwa njia ya Hundi.

## SEHEMU YA NANE

## MATENGO NA MGAO WA ZIADA

Mfuko wa Matengo ya Kisheria

35. Matengo ya mfuko wa kisheria na matumizi yake yatafanywa kwa kuzingatia Kanuni ya 68 ya Vyama vya Ushirika ya Mwaka 2015.

Mfuko wa Elimu na mafunzo

36. Matengo ya mfuko wa elimu na mafunzo pamoja na matumizi yake yatafanywa kwa mujibu wa Kanuni ya 69 ya Vyama vya Ushirika ya Mwaka 2015.

Mgawo wa ziada halisi

37. (1) Ziada halisi ya mwaka pamoja na kiasi chochote kilichopo kwa ajili ya kugawana kutoka miaka iliyopita baada ya taarifa ya fedha kukaguliwa na mkaguzi aliyeidhinishwa na baada ya matengo ya kisheria kufanyika, kiasi kilichobaki kitatumika kwa mujibu wa Kanuni ya 67 ya Vyama Vya Ushirika ya Mwaka 2015 kama ifuatavyo:-

(a) Asilimia isiyopungua ishirini (20%) ya malimbikizo ya ziada kwa mwaka mmoja zitapaswa kutengwa kama fedha taslimu na kuwekwa katika Fungu la Akiba ya Lazima kwa ajili ya kuendeleza chama;

(b) Angalau asilimia kumi na tano (15%) itatengwa katika fedha taslimu kwa ajili ya kukombolea mikopo mibaya na yenye mashaka ikizingatiwa kuwa akaunti hiyo haijazidi asilimia kumi na tano ya madeni yote ya chama;

(c) Asilimia kumi na tano (15%) itatengwa katika fedha taslimu kwa ajili ya Mfuko wa Kukombolea Hisa ilimradi mfuko huo hauzidi asilimia hamsini ya mtaji tete au mtaji msingi, ambacho kitatumika kununulia hisa za wanachama wanaojitoa au kufutwa uanachama; na

(d) Bakaa ya ziada halisi ya mwaka inaweza kugawanywa kama itakavyoamuliwa na Mkutano Mkuu kwa shughuli zifuatazo baada ya

kuidhinishwa na Mrajis:-

i) Kwa ajili ya kulipia faida juu ya Hisa;

ii) Gawio la ziada kwa wanachama;

iii) Zawadi kwa Bodi na watumishi wa kujitolea;

iv) Kuchangia mifuko ya maendeleo kama itakuwepo;

v) Kuchangia shughuli za hisani katika jamii; na

vi) Mambo mengine kama itakavyoamuliwa na Mkutano Mkuu kwa kuzingatia kifungu cha 79 cha Sheria na. 6 ya Vyama vya Ushirika ya Mwaka 2013.

(2) Kwa madhumuni ya kutekeleza Aya ya (v) ya sharti dogo la (1) (d) hapo juu chama kitaanzisha na kutunisha Mfuko Maalumu kwa ajili ya kuchangia shughuli za hisani.

## SEHEMU YA TISA

## USIMAMIZI NA UONGOZI WA CHAMA

Mamlaka ya Mkutano Mkuu

38. (1) Mkutano Mkuu wa wanachama utakuwa na mamlaka ya juu katika kuamua, kuongoza na kusimamia shughuli zote za maendeleo ya chama.

(2) Madaraka ya juu ya chama yatakuwa mikononi mwa wanachama waliohudhuria na kupiga kura katika Mikutano Mikuu.

(3) Kutakuwa na aina tatu za mikutano mikuu ambayo ni mkutano Mkuu wa Mwaka, Mkutano Mkuu wa Kawaida na Mkutano Mkuu Maalum.

Mkutano Mkuu wa Mwaka

39. (1) Mkutano Mkuu wa Mwaka utapaswa kufanyika ndani ya miezi tisa baada ya kufungwa kwa mwaka wa fedha wa chama uliotangulia.

(2) Kwa kuzingatia Kanuni ya 42 ya Vyama vya Ushirika ya Mwaka 2015, masuala yatakayofanyika katika Mkutano Mkuu wa Mwaka ni pamoja na:-

a) Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa Mkutano Mkuu uliopita;
b) Kupokea na kujadili wanachama wapya, waliojitoa, au waliosimamishwa uanachama;
c) Kupokea na kujadili hesabu zilizokaguliwa, taarifa ya ukaguzi, Menejimenti pamoja na taarifa ya ukaguzi ya Mrajis;
d) Kupokea na kujadili taarifa ya Bodi itakayowasilishwa na Mwenyekiti, Kamati ya Mikopo na Kamati ya Usimamizi;
e) Kujadili namna ya kugawa ziada kwa mujibu wa Sheria ya Vyama Vya Ushirika, Na.6 ya mwaka 2013 na Kanuni zake pamoja na Masharti

haya;

f) Kujadili na kuidhinisha mpango mkakati, mpango wa biashara wa chama na program ya utekelezaji na kutathimini utekelezaji wake;

g) Kuweka na kuidhinisha viwango vya Ada na michango mbalimbali;

h) Kuteua Mkaguzi wa Nje kwa ajili ya ukaguzi wa hesabu za chama kwa mwaka unaofuata;

i) Kujadili na kupitisha kiwango cha zawadi (Honoraria) kwa Bodi na watumishi wanaojitolea kadiri itakavyoonekana inafaa;

j) Kujadili na kuidhinisha bajeti ya mapato na matumizi ya chama kwa mwaka unaofuata;

k) Kujadili na kuweka ukomo wa madeni kwa mwaka unaofuata;

l) Kujadili na kukubaliana Kuweka kiwango cha riba ya mikopo na faida juu ya Akiba na Amana;

m) Kujadili na kuidhinisha mipango ya uwekezaji ya Chama;

n) Kujadili na kuazimia rufaa za wanachama; na

o) Kujadili mambo mengineyo yote yahusuyo maendeleo ya chama.

Mkutano Mkuu wa Kawaida

40. (1) TPS SACCOS LTD inaweza kufanya Mkutano Mkuu wa Kawaida angalau mara moja kwa mwaka.

(2) Mambo yatakayozungumzwa katika Mkutano Mkuu wa Kawaida ni pamoja na:-

a) Kusoma na kuthibitisha mambo ya mkutano uliopita;

b) Kujadili na kuidhinisha ununuzi na/au uuzaji wa mali ya chama

inayohamishika au isiyohamishika inayozidi shilingi milioni tano (Shs. 5,000,000/=);

c) Kufanya marekebisho ya Masharti inapoonekana haja ya kufanya hivyo;

d) Kuweka na kuidhinisha idadi ya Wajumbe wa Bodi;

e) Kutafakari namna ya kuitekeleza Sera ya Maendeleo ya Ushirika;

f) Kujadili na kuidhinisha mikataba inayoingiwa na chama;

g) Kuthibitisha wanachama wapya na kuchukua hatua za kinidhamu kwa wanachama wakorofi;

h) Kuchagua au kuwafukuza Wajumbe wa Bodi na wa Kamati ya Usimamizi;

i) Kuchagua wajumbe wa kukiwakilisha chama katika Vyama na Taasisi nyingine zinazohusika na maendeleo ya chama;

j) Kujadili na kupitisha utaratibu wa kazi na kutathmini shughuli za utendaji ili kuleta ufanisi; na

k) Kujadili mambo mengineyo yanayohusu maendeleo ya Chama.

(3) Bila kujali matakwa ya sharti dogo (1) mambo ya Mkutano Mkuu wa Kawaida yanaweza kujumuishwa na kujadiliwa pamoja na mambo ya Mkutano Mkuu wa Mwaka katika Mkutano Mkuu wa Mwaka.

Mkutano ,Mkuu Maalumu

41. (1) Kutakuwepo na Mkutano Mkuu Maalum wakati wowote unapohitajika ambao unaweza kuitishwa na:-

a) Mrajis wa Vyama vya Ushirika au Afisa yeyote aliyeidhinishwa naye;

b) Wanachama; kwa maombi ya maandishi ya wanachama wasiopungua theluthi moja (1/3) ya wanachama wote ambayo ni lazima yaeleze jambo litakalozungumzwa, yawekwe saini au alama ya dole gumba na

waombaji, yaambatishwe na nakala za vitambulisho vya waombaji na nakala ya maombi hayo yatumwe kwa Afisa Ushirika wa Wilaya, Mrajis Msaidizi wa Mkoa na Mrajis; na

c) Wajumbe wa Bodi ya Uongozi ya TPS SACCOS LTD.

(2) Mkutano Mkuu Maalumu utakaoitishwa na wanachama au Bodi ya TPS SACCOS LTD utakuwa na agenda moja tu.

(3) Mkutano Mkuu Maalumu utakaoitishwa na Mrajis au Afisa aliyeidhinishwa naye utaongozwa na Mrajis mwenyewe au mwakilishi wake na ataelekeza mambo yatakayojadiliwa.

Notisi ya Mkutano Mkuu

42. (1) Notisi ya Mkutano Mkuu lazima ioneshe bayana tarehe, saa na mahali pa kufanyia mkutano pamoja na mambo yatakayojadiliwa na itapaswa kubandikwa katika ofisi ya Chama na kwenye mbao za matangazo.

(2) Bodi ya Uongozi inaweza kutumia njia nyingine za mawasiliano kama simu, barua pepe, Runinga au matangazo ya redio katika kuhakikisha notisi ya Mkutano Mkuu inawafikia wajumbe wa mkutano mkuu kwa wakati.

(3) Muda wa notisi ya Mkutano Mkuu utakuwa:-

i) Kwa Mkutano Mkuu wa Mwaka na Mkutano Mkuu wa Kawaida siyo chini ya siku ishirini na moja (21) kabla ya tarehe ya kufanyika mkutano; na

ii) Kwa Mkutano Mkuu Maalum siyo chini ya siku saba (7).

Akidi ya Mkutano Mkuu

43. (1) Akidi katika Mkutano Mkuu yote, isipokuwa Mkutano Mkuu Maalumu ulioitishwa na Mrajis, itakuwa si chini ya nusu (1/2) ya wanachama wote au wanachama mia moja (100) ikichukuliwa idadi yoyote iliyo ndogo.

(2) Ikiwa katika Mkutano Mkuu wa mwaka au katika Mkutano Mkuu wa kawaida, Akidi kama haijatimia baada ya kupita muda wa saa moja wa kusubiri tangu muda uliopangwa kuanza Mkutano, Mwenyekiti wa Bodi ataahirisha mkutano huo kwa muda wa siku saba na utakapoitishwa tena mambo yatakayozungumzwa yatakuwa yale ya mkutano ulioahirishwa.

(3) Endapo Mkutano Mkuu ulioahirishwa umeitishwa baada ya siku saba na akidi haikutimia baada ya kupita muda wa kusubiri uliopangwa kuanza mkutano, mkutano huo utafutwa na taarifa kupelekwa kwa Mrajis.

(4) Mkutano Mkuu Maalum ulioitishwa na Mrajis au mwakilishi wake utafanyika kwa muda uliopangwa hata kama akidi haijatimia na maazimio yatakayopitishwa katika mkutano huo yatakuwa halali.

Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu

44. Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu, isipokuwa Mkutano Mkuu Maalum ulioitishwa na Mrajis, atachaguliwa na wanachama katika kila Mkutano Mkuu na atahudumu kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 40 ya Vyama vya Ushirika ya Mwaka 2015.

Upigaji Kura katika Mkutano Mkuu

45. (1) Mwanachama yeyote ambaye ametimiza masharti ya uanachama kama ilivyo katika masharti haya atakuwa na kura moja katika Mkutano Mkuu wa chama na hakutakuwa na kura ya uwakilishi.

(2) Maazimio ya Mkutano Mkuu yatafanywa kwa kupiga kura ya kunyoosha mikono isipokuwa kama kura ya siri itahitajika na kuungwa mkono na wanachama wasiopungua nusu (1/2) ya wajumbe waliohudhuria kwenye Mkutano huo;

(3) Katika Mkutano Mkuu maamuzi ya wengi yatachukuliwa na endapo kura zitalingana jambo hilo litarudiwa kupigiwa kura au kusubiri mkutano utakaofuata.

Muhtasari wa Mkutano Mkuu

46. (1) Kumbukumbu za masuala yote yaliyojadiliwa, kuamuliwa au kuazimiwa katika Mkutano Mkuu zitaandaliwa na kusainiwa na Katibu wa

Mkutano na baada ya kuthibitishwa katika mkutano unaofuata kumbukumbu hizo zitasainiwa na Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu na kutunzwa katika kitabu cha kumbukumbu za mikutano.

(2) Bodi ya Uongozi ya TPS SACCOS LTD itapaswa kutuma nakala ya muhtasari uliyothibitishwa kwa Mrajis ndani ya siku thelathini tokea tarehe ya Mkutano Mkuu uliothibitisha muhtasari husika.

## SEHEMU YA KUMI

## BODI YA UONGOZI NA KAMATI YA USIMAMIZI

Bodi ya Uongozi

47. (1) Kutakuwa na Bodi ya Uongozi ya TPS SACCOS LTD ambayo itakuwa na wajumbe wasiopungua watano (5) na wasiozidi tisa (9) akiwemo Mwenyekiti na Makamu wake.

(2) Bila kuathiri matakwa ya sharti dogo la (1) Mkutano Mkuu unaweza kuweka idadi nyingine ya Wajumbe wa Bodi ya Uongozi kwa kuzingatia mahitaji ya shughuli za chama kwa wakati uliopo.

(3) Wajumbe wa Bodi ya Uongozi ya TPS SACCOS LTD watachaguliwa na Mkutano Mkuu kwa kuzingatia Sheria na.6 ya Vyama vya Ushirika ya Mwaka 2013 pamoja na Kanuni zake.

(4) Wajumbe wa Bodi ya Uongozi watahudumu katika nafasi hiyo kwa awamu moja ya kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuchaguliwa kuhudumu tena kwa awamu nyingine ya kipindi cha miaka mitatu na baada ya hapo hawataruhusiwa/hawatakuwa na sifa ya kugombea kwa awamu nyingine moja itakayofuatia.

(5) Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi na Makamu wake watachaguliwa na Mkutano Mkuu kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Bodi.

(6) Kutakuwa na uwakilishi kutoka katika kila ngazi ya wilaya/mkoa/kanda ambao watakuwa wajumbe wa baraza la wawakilishi(mkutano mkuu wa wanachama) kama itakavyoainishwa katika sera ya uwakilishi:

Kukoma Ujumbe wa Bodi;

48. Mjumbe wa Bodi ya TPS SACCOS LTD atakoma kuwa mjumbe,

endapo:-

a) Ameacha kuwa mwanachama wa chama;

a) Amepatwa na kichaa cha kudumu kilichothibitishwa na daktari wa hospitali inayotambulika kisheria;

b) Atatumia ofisi ya chama kwa manufaa yake binafsi;

c) Kifo;

d) Atafanya shughuli zozote zinazofanana na shughuli za chama na wanachama au watu ambao wanaweza kuwa wanachama wa TPS SACCOS LTD;

e) Atafukuzwa na Mkutano Mkuu kwa azimio lililoungwa mkono na idadi ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wasiopungua nusu (1/2) ya wajumbe waliohudhuria kwenye Mkutano huo;

f) Kwa kushindwa kuhudhuria vikao vya Bodi vitatu mfululizo bila sababu za msingi.

Vikao vya Bodi ya Uongozi

49. (1) Vikao vya Bodi ya Uongozi vitafanyika mara nne kwa mwaka na pale itakapohitajika Bodi inaweza kufanya vikao vya dharura viwili.

(2) Bodi ya Uongozi itapaswa kuandaa ratiba ya vikao vya Bodi na kuiwasilisha kwa Mrajis na Mrajis Msaidizi wa Mkoa.

(3) Mwenyekiti wa Bodi ataongoza kikao cha Bodi na endapo hatakuwepo, Makamu Mwenyekiti ataongoza kikao hicho na iwapo wote wawili hawatakuwepo katika kikao hicho, mjumbe wa Bodi mwingine yeyote kati ya waliohudhuria atachaguliwa kuwa Mwenyekiti wa muda na ataongoza kikao hicho.

(4) Vikao vya Bodi vitakuwa ni halali iwapo wajumbe waliohudhuria ni nusu ya wajumbe wote.

(5) Kila mjumbe wa Bodi atakuwa na kura moja na iwapo kura zitalingana, Mwenyekiti atakuwa na kura ya ziada.

Muhtasari wa Vikao vya Bodi ya Uongozi

50. Kumbukumbu za masuala yote yaliyojadiliwa, kuamuliwa au kuazimiwa katika vikao vya Bodi zitaandaliwa na kusainiwa na katibu na baada ya kuthibitishwa katika kikao kinachofuata, kumbukumbu hizo zitasainiwa na Mwenyekiti wa Bodi na kutunzwa katika kitabu cha kumbukumbu za vikao vya Bodi.

Kazi za Bodi ya Uongozi

51. (1) Kwa kuzingatia Kanuni ya 24 ya Huduma Ndogo za Fedha ya SACCOS ya Mwaka 2019 na Kanuni ya 51 ya Vyama vya Ushirika ya Mwaka 2015, Bodi ya Uongozi itakuwa na wajibu wa kusimamia shughuli za kila siku za chama.

(2) Bila kuathiri matakwa ya sharti dogo (1) Bodi ya chama itapaswa kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kusimamia shughuli zote za Chama na kuhakikisha kuwa zinaendeshwa ipasavyo;

(ii) Kutekeleza kikamilifu maazimio na maelekezo ya Mkutano Mkuu;

(iii)Kuandaa na kutunza Hesabu za Chama kwa usahihi na kwa wakati;

(iv)Kutunza kwa usahihi daftari la wanachama na kumbukumbu za mihtasari ya Mikutano Mikuu na Vikao vya Bodi;

(v) Kuhakikisha kuwa lakiri ya chama inakuwepo na inatumika ipasavyo;

(vi)Kufanya maamuzi kuhusu udahili wa wanachama wapya, kujiuzulu wanachama, kusimamishwa uanachama na kusimamishwa kwa wajumbe wa Bodi na kuwasilisha masuala hayo kwenye Mkutano Mkuu kwa ajili ya kujadiliwa na kutolewa maamuzi ya mwisho;

(vii) Kubuni na kutayarisha Sera na kanuni mbalimbali

zinazohusiana na shughuli za chama ili kufanikisha madhumuni ya chama.

(viii) Kuandaa na kuwasilisha kwenye Mkutano Mkuu taarifa ya hali ya uchumi na maendeleo ya chama pamoja na hesabu ya mapato na matumizi, mizania iliyothibitishwa kwa mwaka uliopita na makisio ya mapato na matumizi kwa mwaka unaofuata;

(ix) kupokea na kujadili taarifa za Kamati ya Mikopo na Kamati ya Usimamizi na kufanyia kazi ushauri na mapendekezo yaliyotolewa kikamilifu na kwa wakati;

(x) Kupitia, kujadili na kutolea maamuzi maombi ya mikopo kutoka kwa Wajumbe wa Bodi, Wajumbe wa Kamati ya Mikopo na Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi;

(xi) Kuteua mwanachama atakayeshika nafasi iliyoachwa wazi katika Kamati ya Mikopo na mjumbe aliyeteuliwa atashika nafasi hiyo mpaka Mkutano Mkuu mwingine unaofuata ambapo nafasi iliyoachwa wazi itajazwa kwa kupigiwa kura au kwa uthibitisho;

(xii) Kumwezesha mtu aliyeidhinishwa kukagua vitabu vya chama na kuhakikisha kuwa hatua zinachukuliwa kutokana na Taarifa ya ukaguzi;

(xiii) Kuhakikisha kuwa wanachama wanafuata na kuzingatia Masharti haya, taratibu, mikataba na miongozo mbalimbali;

(xiv) Kufungua akaunti Benki na kuhakikisha kuwa fedha zote za chama zinatunzwa katika benki;

(xv) Kujadili na kuweka mipango ya namna ya kutekeleza Sera ya Maendeleo ya Ushirika;

(xvi) Kuandaa mpango mkakati, mpango wa biashara na programu

ya utekelezaji wake;

(xvii) Kuhakikisha kwamba chama kinawakilishwa katika mashitaka yoyote;

(xviii) Kuhakikisha kuwa mali, bidhaa, vifaa na nyaraka/Hati za Chama zinahifadhiwa vizuri na kwa usalama;

(xix) Kuteua watia saini kwenye hundi za chama;

(xx) Kuajiri na kuteua watumishi wenye sifa za kutosha kutenda shughuli za Chama wakiwemo Meneja, Mhasibu Hazina au watumishi wengine miongoni mwa wanachama au nje ya wanachama ambao wataendesha shughuli za kila siku za chama;

(xxi) Kuingia mikataba mbalimbali kwa niaba ya chama kwa kuzingatia kanuni ya 76 ya Kanuni za Vyama vya Ushirika za mwaka 2015;

(xxii) Kuhakikisha kuwa wakopaji wanalipa madeni yao kama walivyoahidi na kuwachukulia hatua za kisheria wakopaji wasio waaminifu;

(xxiii) Kupendekeza kwenye Mkutano Mkuu ufutaji wa mikopo mibaya ambayo haiwezi kulipwa kabisa.

(xxiv) Kupendekeza kwenye Mkutano Mkuu mabadiliko au viwango vya riba au masharti ya ulipaji mikopo au mgawanyo wa mikopo (amortization);

(xxv) Kuandaa marekebisho ya masharti ya chama pale itakapobidi na kuwasilisha kwenye Mkutano Mkuu kwa ajili ya kujadiliwa na kutolewa maamuzi;

(xxvi) Kuwasilisha kwa Mrajis mikataba yote ya kibiashara

iliyoingiwa na chama kwa ajili ya kusajiliwa;

(xxvii) Kusimamia utekelezwaji wa shughuli za chama kwa kumtaka Meneja/Katibu kutoa taarifa ya matokeo ya uendeshaji wa shughuli za chama;

(xxviii) Kuchapisha Hati za kumiliki hisa kwa ajili ya wanachama;

(xxix) kuandaa mipango ya uwekezaji na kuiwasilisha kwenye Mkutano Mkuu kwa ajili ya kujadiliwa na kutolewa maamuzi;

(xxx) Kufanya mambo mengine yote ambayo yataonekana ni lazima katika kutimiza madhumuni ya chama kwa kuzingatia Sheria za nchi.

Kazi za Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi

52. Mwenyekiti wa Bodi atapaswa kutekeleza kazi zifuatazo:-

a) Kuongoza vikao vyote vya Bodi ya Chama;

b) Kwa kushirikiana na Katibu kuitisha Mikutano Mikuu na vikao vya Bodi kwa kuzingatia Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013, Kanuni zake na Masharti haya;

c) Kutia saini kumbukumbu za vikao vya Bodi;

d) Kutia saini kwa niaba ya Chama, kumbukumbu zote ikiwa ni pamoja na zinazohitaji kuwekwa lakiri na/au muhuri wa Chama;

e) Kuwa msemaji mkuu wa Chama, kama haitaamriwa vinginevyo na Bodi au Mkutano Mkuu wa wanachama.

Kazi za Makamu Mwenyekiti

53. Makamu Mwenyekiti atapaswa kutekeleza kazi zote za Mwenyekiti endapo Mwenyekiti hatakuwepo.

Sifa za Mjumbe wa Bodi ya Uongozi na Mjumbe wa Kamati ya Usimamizi

54. Mjumbe wa Bodi ya Uongozi na wa Kamati ya Usimamizi lazima awe na sifa zifuatazo:-

a) Awe na elimu ya angalau ya kiwango cha stashahada ya uongozi au uhasibu au biashara au elimu inayolingana nayo;

b) Awe amekuwa mwanachama si chini ya mwaka mmoja isipokuwa wakati wa kuanza chama;

c) Awe mwadilifu na mwaminifu;

d) Awe na uwezo wa kuongoza;

e) Awe ametimiza matakwa ya sharti la 15 (1) (b) na 15 (2) la Masharti haya kuhusu ulipaji wa hisa;

f) Awe hajawahi kupoteza sifa za uongozi katika ngazi yoyote ya Chama cha Ushirika;

g) Awe hajawahi kuwa mjumbe wa Bodi iliyoshindwa kusimamia vizuri shughuli za chama na kikapata hasara;

h) Awe anashiriki kikamilifu katika shughuli zote za chama.

i) Hajawahi kusababisha hasara katika chama chochote cha ushirika;

j) Asiwe na tabia ya kulaza madeni; na

k) Awe amethibitishwa kazini.

Kazi za Meneja

55. (1) Meneja wa TPS SACCOS LTD atakuwa na wajibu wa kusimamia utekelezwaji wa shughuli za kila siku za chama ambazo zitajumuisha:-

(a) kutekeleza na kuzingatia Sheria ya Vyama vya Ushirika na Kanuni zake, Sera ya Maendeleo ya Ushirika, Masharti haya, Kanuni na Sera mbalimbali zilizowekwa kwa ajili ya kuongoza utekelezaji wa shughuli za chama;

(b) Kuhakikisha mifumo ya utendaji na utoaji taarifa ipo madhubuti na inawezesha mawasiliano;

(c) Kwa kushauriana na Wajumbe wa Bodi, kuandaa mpango mkakati, mpango biashara, bajeti ya mwaka na program ya utekelezaji;

(d) Kuhakikisha malengo na shabaha za chama zinafikiwa;

(e) Kushughulikia masuala yote yanayowahusu watumishi, hususan mafunzo na uendelezaji wa rasilimali watu;

(f) Kwa kushirikiana na Wajumbe wa Bodi, kuiwakilisha TPS SACCOS LTD katika shughuli na uingiaji wa mikataba;

(g) Kuhakikisha vitabu vya hesabu vinaandikwa na hesabu zinaandaliwa na kuwasilishwa kwa Wakaguzi kwa wakati;

(h) Atahakikisha taarifa ya mapato na matumizi, mizania, na taarifa ya mikopo iliyochelewa zimeandaliwa kwa usahihi na wakati;

(i) Kutoa taarifa za menejimenti kwenye vikao vya Bodi ambazo zinaelezea hali ya kifedha ya TPS SACCOS LTD ikianisha mizania, hesabu ya mapato na matumizi, taarifa ya mikopo iliyochelewa, bajeti ya mwaka, mwenendo wa chama na uwiano wake;

(j) Kuidhinisha matumizi yaliyoko kwenye makisio kwa viwango vilivyowekwa na Bodi na kutia saini kwenye nyaraka zinazoruhusu utoaji fedha za chama kwa kuzingatia ukomo ulioainishwa kwenye sera za chama;

(k) Kuisaidia Bodi kupanga viwango stahiki vya riba, ada na gharama nyingine kwa bidhaa na huduma zitakazotolewa;

(l) Kuisaidia Bodi katika kubainisha dhamana zinazokubalika na zinazoweza kutumika kudhamini mikopo;

(m) Kuhakikisha kuwa kuna ukwasi wa kutosha kukidhi mahitaji ya mikopo, uchukuaji wa akiba na gharama za uendeshaji;

(n) Kusimamia ufunguaji na uendeshaji wa akaunti;

(o) Kutoa taarifa stahiki kwa mamlaka zinazohusika kwa muda muafaka;

(p) Kutekeleza mapendekezo yanayotolewa kwenye taarifa za Wakaguzi wa Ndani na wa Nje na taarifa za kiuchunguzi zinazotolewa na mamlaka husika; na

(q) Kufanya kazi na majukumu mengine kadri ya maelekezo ya Bodi.

(2) Katika kutekeleza majukumu yake yaliyoainishwa katika sharti dogo la (1), Meneja atawajibika kwa Bodi.

Kamati ya Usimamizi

56. (1) Kutakuwa na Kamati ya Usimamizi ya chama ambayo itakuwa na wajumbe wasiozidi watatu watakaochaguliwa na Mkutano Mkuu na hawapaswi kwa wakati mmoja kuwa Wajumbe wa Bodi, au Wajumbe wa Kamati ya Mikopo au waajiriwa wa chama.

(2) Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi watahudumu katika nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.

(3) Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi watachagua Mwenyekiti na Katibu kutoka miongoni mwao. Katibu atatunza kumbukumbu zote za vikao vya Kamati ya Usimamizi.

Kazi za Kamati ya Usimamizi

57. Kamati ya Usimamizi itapaswa kutekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Kufanya mapitio ya mara kwa mara kuhusu usahihi wa kumbukumbu za hesabu;

(b) Kutoa taarifa kwenye kila kikao cha kawaida cha Bodi;

(c) Kutoa mapendekezo ya kuboresha Sera, taratibu za uendeshaji na udhibiti wa ndani na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wake;

(d) Kuandaa taarifa ya ukaguzi na usimamizi wa hesabu ya mwaka na kuiwasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa mwaka kama Mkaguzi wa nje hataweza kufanya hivyo;

(e) Kupendekeza kwa Bodi wakaguzi wa nje watakaofanya ukaguzi kwa mwaka wa fedha unaofuata;

(f) Kusimamia fedha na mali zote za chama kwa niaba ya wanachama.

(g) Kufuatilia maendeleo ya miradi mikubwa ya wanachama ambayo imepatiwa mkopo na chama mpaka wahusika wanapomaliza marejesho.

(h) Kutafuta ufumbuzi wa masuala mbalimbali ya kiuongozi na kushauri Mkutano Mkuu ipasavyo; na

(i) kutekeleza majukumu mengine kwa mujibu wa Sheria ya Vyama Vya Ushirika na Kanuni zake pamoja.

Kamati ya Mikopo

58. Kutakuwa na Kamati ya Mikopo itakayokuwa na Wajumbe watatu, ambao watachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Mwaka au watateuliwa na Bodi kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Bodi ya Uongozi na watapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-

(a) Uzoefu katika masuala ya mikopo;

(b) Uwezo wa kufanya uchambuzi wa hali na mtiririko wa fedha za mwanachama;

(c) Ufahamu kuhusu uanachama;na

(d) Ufahamu na uelewa wa shughuli za eneo husika na mazingira ya kiuchumi.

(2) Kamati ya mikopo inaweza kukasimisha sehemu au mamlaka yake yote ya uidhinishaji wa mikopo, kwa kamati ya kitaalam ya mikopo ambayo inaweza kuundwa na waajiriwa na maafisa wa TPS SACCOS LTD.

(3) Kamati ya kitaalamu ya mikopo itakuwa na wajumbe wasiozidi watano.

(4) Pale ambapo mamlaka ya uidhinishaji wa mikopo yamekasimishwa kwa Kamati ya kitaalamu ya mikopo, kamati hiyo itapaswa kuandaa muhtasari wa shughuli zake zote zinazohusu mikopo na kuiwasilisha kwenye vikao vya Bodi vya kawaida.

Wajibu wa Kamati ya Mikopo au Kamati ya Kitaalamu

59. (1) Kamati ya Mikopo au Kamati ya Kitaalamu itapaswa:-

(a) Kukutana mara kwa mara kuzingatia ukubwa wa shughuli zake kwa ajili ya kupitia na kutoa maamuzi, ila isipungue kikao kimoja kwa kila robo mwaka na maamuzi yatafanywa kwa wingi wa kura za Wajumbe wa Kamati na yatawekwa kama kumbukumbu ya kikao;

(b) Kutoa ushauri kwa wanachama kuhusu ukopaji na matumizi ya mikopo kwa busara;

(c) Kufanya mapitio ya maombi ya mikopo na kuyatolea maamuzi kwa kuzingatia kikomo cha mamlaka ya Kamati na sera ya mikopo;

(d) Kuhakikisha kwamba dhamana ya kutosha imewekwa kwa kila mkopo na kwamba TPS SACCOS LTD inakuwa na udhibiti wa dhamana husika hadi mkopo wote utakaporejeshwa;

(e) Kufanyia kazi maombi ya mwanachama kuhusu marekebisho kwenye vigezo na masharti ya mkopo ilimradi tu marekebisho hayo

yanalandana na sera ya mikopo ya TPS SACCOS LTD;

(f) Kuhakikisha kuwa mikopo inatumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa;

(g) Kutoa kipaumbele kwa maombi ya mikopo yenye kiwango kidogo kama mahitaji na masharti ya mkopo yako sawa, iwapo fedha zilizopo hazitoshelezi kukidhi maombi yote ya mikopo yaliyowasilishwa; na

(h) Kufanya shughuli nyingine kwa mujibu wa Sheria ya Vyama Vya Ushirika na Kanuni zake.

(2) Mamlaka ya ukopeshaji na mazuio yoyote kuhusu Kamati ya Mikopo au Kamati ya kitaalamu ya mikopo yataainishwa kwenye sera ya mikopo.

(3) Haitaruhusiwa katika mazingira yoyote kwa mtu kuidhinisha maombi ya mkopo wake mwenyewe.

Akidi ya Vikao vya Kamati ya Mikopo

60. Vikao vya Kamati ya Mikopo vitakuwa halali pale vitakapokuwa na mahudhurio ya wajumbe wasiopungua wawili (2).

Rufaa dhidi ya maamuzi ya Kamati

61. Mwanachama wa TPS SACCOS LTD anaweza kukata rufaa kwa maandishi, dhidi ya maamuzi yaliyofanywa na Kamati ya Kitaalamu kwa Kamati ya Mikopo na maamuzi yaliyofanywa na Kamati ya Mikopo kwa Bodi ya Uongozi ambayo maamuzi yake yatakuwa ya mwisho.

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA

## UANDAAJI WA SERA NA MIONGOZO YA CHAMA

62. Chama kitaandaa sera na miongozo mbalimbali kama ilivyoelekezwa kwenye kanuni ya vyama vya ushirika. Miongozo hiyo ni pamoja na:-

Chama kuandaa Sera na miongozo

i. Sera ya mikopo
ii. Sera ya uhifadhi kumbukumbu
iii. Sera ya ukwasi
iv. Sera ya uhamasishaji Hisa na Akiba
v. Sera ya uwekezaji
vi. Mwongozo wa usimamizi wa majanga
vii. Sera ya udhibiti wa ndani
viii. Sera ya utumishi
ix. Kanuni za fedha
x. Mpango mkakati

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI

## KUFUTWA NA UFILISI WA CHAMA

Sababu za kufutwa

63. (1) TPS SACCOS LTD inaweza kufutwa:-

i. Kwa amri ya Mrajis wa Vyama vya Ushirika; na

ii. Kwa maombi ya wanachama wasiopungua robo tatu (3/4) ya wanachama wote.

Ufilisi

64. (1) Ufilisi wa TPS SACCOS LTD utafanywa kwa kufuata utaratibu kama ulivyoainishwa chini ya Sheria.

(2) Pale ambapo Mfilisi atakuwa amekamilisha ufilisi na kuwa amewalipa wadai wote wa chama, bakaa ya fedha za chama zitagawiwa kwa waliokuwa wanachama wa TPS SACCOS LTD wakati wa kufutwa kwake kwa uwiano ulio sawa.

## SEHEMU YA KUMI NA TATU

## MASHARTI MENGINEYO

Viongozi kutunza siri

65. Wajumbe wa Bodi, Watendaji Wakuu na watumishi wa TPS SACCOS LTD watapaswa kutunza **SIRI** kuhusu kumbukumbu zote za maisha ya mwanachama binafsi, isipokuwa masuala ya utoaji na ukusanyaji wa mikopo ambayo Bodi inaweza kuchukua hatua zozote za lazima dhidi ya walipaji wasiokuwa waaminifu.

TPS SACCOS LTD kuungana na ţaasisi nyingine

66. (1) TPS SACCOS LTD inaweza kuungana na chama kingine cha ushirika kuanzisha Mradi wa Pamoja wa Ushirika au kuungana na kampuni au taasisi nyingine isiyo ya Ushirika kuanzisha Ubia wa Pamoja.

(2) TPS SACCOS LTD kinaweza kuungana na Vyama vingine na kuunda Chama Kikuu cha Ushirika.

Bima ya mali na fedha za chama

67. TPS SACCOS LTD itakuwa na wajibu kuhakikisha usalama wa mali na fedha kwa kukata bima.

Mabadiliko ya Masharti

68. Masharti haya yanaweza kubadilishwa kwa kufuata taratibu zilizowekwa na Sheria ya Vyama Vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 na Kanuni zake na hayatakuwa halali kutumika mpaka yatakapoidhinishwa na kusajiliwa na Mrajis wa Vyama Vya Ushirika.

Utatuzi wa migogoro

69. (1) Mgogoro wowote unaohusu shughuli za TPS SACCOS LTD kati ya wanachama wake au watu wanaowalalamikia, au kati ya mwanachama au watu ambao wanadai na Bodi au Afisa yeyote, au kati ya TPS SACCOS LTD na chama cha ushirika kingine au Mtoa Huduma utasuluhishwa kwa njia ya amani kupitia majadiliano au maridhiano.

(2) Ikiwa mgogoro chini ya sharti dogo la (1) haujasuluhishwa kwa amani ndani ya siku 30, mgogoro huo utapelekwa kwa Mrajis kwa usuluhishi kupitia Fomu Na. 13 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2015.

(3) Kupelekwa kwa usuluhishi chini ya sharti dogo la (2) kunaweza kufanywa na Bodi au TPS SACCOS LTD kwa azimio la Mkutano Mkuu au na mhusika yeyote katika mgogoro au na mwanachama yeyote wa TPS SACCOS LTD kama mgogoro unamhusu Mjumbe wa Bodi kudaiwa kiasi cha fedha na chama.

(4) Katika kupeleka mgogoro kwa Mrajis chini ya sharti dogo la (3), mlalamikaji atapaswa kupeleka nakala ya marejeo kwa ajili ya mlalamikiwa.

(5) Katika kupokea marejeo chini ya sharti dogo la (2), Mrajis ataweka tarehe ya kupokea na kutuma nakala kwa mlalamikiwa na wahusika wote ambao kwa maoni yake mgogoro huo unawahusu.

(6) Baada ya kupokea marejeo ya mgogoro katika sharti dogo la (5), mlalamikiwa atapaswa ndani ya siku kumi na tano tokea tarehe ya kupokea, kuwasilisha maelezo ya kujibu kwa Mrajis.

Mgongano wa tafsiri ya Masharti

70. Endapo kutatokea mgongano kuhusu tafsiri ya Masharti haya, suala hili litapelekwa kwa Mrajis wa Vyama Vya Ushirika kwa ajili ya maamuzi.

Utakatishaji wa fedha

72 Chama kitaandaa miongozo na taratibu za ndani kwa ajili ya kubaini na kutoa taarifa dhidi ya vitendo vya utakatishaji wa fedha kama inavyoelezwa kwenye sheria ya utakatishaji fedha.

| | | |
|---|---|---|
| Uombaji wa leseni | 73 | Chama kitaomba leseni daraja B kutoka Tume ya Maendeleo ya Ushirika ya kufanya biashara ya huduma ndogo ya fedha kwa mujibu wa sheria ya huduma ndogo za fedha Na. 10 ya mwaka 2018. |
| Ulinzi wa mtaji | 74 | Chama kitapaswa kuweka wazi upatikanaji wa huduma zitolewazo na chama na kuweka utaratibu wa kushughulikia malalamiko yatakayojitokeza. |
| Mihuri ya chama | 75 | Chama kitakuwa na Mihuri ya mpira ambayo itatunzwa na Meneja wa chama na itahifadhiwa kwenye kasiki ya chama. |
| Msemaji wa chama | 76 | Mwenyekiti wa bodi ya uongozi ndiyo atakuwa msemaji wa chama |
| Ulipaji wa riba na Gawio | 77 | Chama kitahakikisha kinalipa riba juu ya akiba kwa amana za wanachama pamoja na kutoa gawio kwa kuzingatia faida iliyopatikana Kwa muda husika. |

## 9.0 HITIMISHO

Masharti haya yametayarishwa na kupitishwa na Bodi ya chama iliyokasimiwa madaraka kwa niaba ya wanachama kwa barua ya mrajis msaidizi wa Mkoa wa Dar es salaam yenye Kumbukumbu Na.MA.82/309/83/20 ya tarehe 02 Oktoba 2020 na yatatumika baada ya kuidhinishwa na Mrajis.

**ORODHA YA MAJINA YA WAJUMBE WALIOANDAA MASHARTI HAYA**

| Na. | Jina la Mwanachama | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 | SACP George T. Mwambashi | | 1 Oktoba 2020 |
| 2 | SSP Stanslaus B. Kagali | | 1 Oktoba 2020 |
| 3 | CP Gideon N. Nkana (rtd) | | 1 Oktoba 2020 |
| 4 | SACP Hamis M. Nkubas (rtd) | | 1 Oktoba 2020 |
| 5 | SP Baraka A. Ulimboka (rtd) | | 1 Oktoba 2020 |
| 6 | SP Yunge M. Saganda | | 1 Oktoba 2020 |
| 7 | S'Sgt Erasto C. Gama | | 1 Oktoba 2020 |

**MWENYEKITI**

……………………

**KATIBU**

……………………

**Mrajis wa vyama vya Ushirika**

**Tarehe…………………………**

TANZANIA
Registered this 01ST
day of MARCH 2021
Asst. Registrar of Cooperative Societies